



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KWA KIPINDI CHA
ROBO YA KWANZA (JULAI-SEPTEMBER) KILICHOFAANYIKA TAREHE 02
NOVEMBA, 2021 KATIKA UKUMBI WA MANISPAA

MAHUDHURIO

a) Wajumbe waliohudhuria

1. Mhe, Fank Magali (Meya)		Mwenyekiti
2. Mhe, Salum B. Ng`ondo	Naibu Meya	Mjumbe
3. Mhe, Khalfan M. Mandanje		Mjumbe
4. Mhe, Nyanga M. Nyanga		Mjumbe
5. Mhe, Asina Kawanga		Mjumbe
6. Mhe, Jumu A. Ndondi		Mjumbe
7. Mhe, Lunda J. Lunda		Mjumbe
8. Mhe, Mwanajuma Amiri		Mjumbe

Wajumbe wasiohudhuria

1. Mhe, Hamida Abdallah (MB)	Kwa taarifa
2. Mhe, Salma Rashid Kikwete (MB)	Kwa taarifa

Wataalam waliohudhuria

1. Ndg.Juma Mnwele	Mkurugenzi wa Manispaa - Mwenyekiti
2. Ndg.Kihanza B.J	Afisa Utumishi wa Manispaa - Katibu
3. Ndg.Tatu O. Seif	Kaimu Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa
4. Ndg.Bakari Ndege	Kaimu Mratibu wa TASAF wa Manispaa
5. Ndg.Raphael Mauna	Mhasibu wa Mapato
6. Ndg.Razaro Shija	Kaimu Mwanasheria wa Manispaa
7. Ndg.Steven Mhina	Afisa Manunuzi na Ugavi wa Manispaa
8. Ndg.Edward Msangi	Kaimu Mweka Hazina wa Manispaa
9. Ndg.Gregory Majawa	Mdhibiti Ubora wa Shule wa Manispaa
10. Ndg.Hussein Mwapili	Kaimu Afisa Kilimo wa Manispaa
11. Ndg.Wilfred Luke	Afisa Ushirika wa Manispaa
12. Ndg.Yusta Msindo	Mchumi
13. Dkt. Ninzar Idd	Afisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa
14. Ndg.Msuka M.P	Kaimu Afisa Ardhi, Mipangomiji na Maliasili wa Manispaa
15. Ndg.Moses J. Mkoveke	Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa

16.Ndg.Ezekiel Magembe
17.Ndg.Mbwana Mbwana

Kaimu Afisa Mazingira na Udhhibiti wa Taka Ngumu
Kaimu Afisa TEHAMA wa Manispaa

Wajumbe wasiohudhuria

Sekretarieti

1.Carlos G. Kanyopa Kaibu wa Kamati

HML/ KF/MUTH; NA 19/2021/2022 KUFUNGA KIKAO

Kabla ya kufungua kikao, Katibu alianza kwa kueleza kuwa, Kikao hicho ni cha kawaida kwa kipindi cha Robo ya Kwanza (Julai-Septemba), 2021/2022 ambacho kitajadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Halmashauri kwa kipindi hicho. Baada ya kusema hayo, alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alianza kwa kuwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria kikao hicho na kuwataka kuchangia kwa mapana kila jambo litakaloletwa mbele ya kikao kwa ajili ya majadiliano. Baada ya kusema hayo, Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:36 Asubuhi.

HML/ KF/MUTH; NA 20/2021/2022 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA AGENDA

1. Kufungua kikao
2. Kupokea na kuthibitisha Agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha Tarehe 24/09/2021
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 24/09/2021
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha Robo ya kwanza Julai-Septemba,) 2021/2022
6. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Shughuli za kawaida kwa kila Idara kwa kipindi cha robo ya kwanza (Julai-Septemba) 2021/2022
7. Taarifa ya Manunuzi na Ugavi kwa Kipindi cha Robo ya kwanza (Julai-Septemba) 2021/2022
8. Taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Sh 1,120,000,000.00 (Fedha za UVIKO 19) kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa ya Shule za Msingi na Sekondari.
9. Taarifa ya Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha Robo ya kwanza Julai-Septemba,) 2021/2022
10. Mengineyo
11. Kufunga Kikao

HML/ KF/MUTH; NA 25/2021/2022 KUPOKEA NA KUIDHINISHA TAARIFA YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KWA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI.

Ilielezwa kuwa serikali kupitia mpango wa maendeleo na mapambano dhidi ya UVIKO - 19 imeipatia halmashauri ya manispaa ya Lindi kiasi cha Tshs. 420,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule za msingi 8 na Tshs.700,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule 21 za sekondari Kwa upande wa shule za msingi

madarasa yanayotarajiwa kujengwa ni 14 ambayo yatajengwa katika shule shikizi na sekondari yatajengwa madarasa 35.

Aidha, orodha ya shule ambazo zitanufaika na fedha hizo iliambatishwa katika tarifa hiyo.

Maoni ya Wajumbe wa Kamati


Baada ya kuwasilishwa, wajumbe walitoa shukrani za dhati kwa Mhe, Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupatiwa fedha hizo kwani zitapunguza msongamano wa wanafunzi katika shule hizo.

Aidha, Mstahiki Meya alisisitiza kuwa fedha hizo zitumike kama zilivyopangwa na kuagiza kuwa miradi hiyo iendane na thamani halisi ya fedha hizo.


Baada ya maoni hayo, wajumbe waliipokea tarifa hiyo na kupitisha matumizi ya fedha hizo.

HML/ KF/MUTH; NA 27/2021/2022 KUFUNGA KIKAO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Mwenyekiti alianza kwa kuwashukuru Wajumbe kwa uvumilivu wao pamoja na michango yao yenye tija. Baada ya kusema hayo alifunga kikao saa 6:42 Mchana.


.....
Juma A. Mnwele
Katibu

UMETHIBITISHWA NA


.....
Frank Magali
Mwenyekiti

Tarehe 02.11.2021